# KITINI CHA UFUGAJI BORA WA KUKU WA ASILI

## KWA KUONGEZA PATO LA KAYA MASKINI

## MRADI WA KUONGEZA THAMANI KATIKA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI (AVA)



Funded by the European Union

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

MJUMITA

# KITINI CHA UFUGAJI BORA WA KUKU WA ASILI

# KWA KUONGEZA PATO LA KAYA MASKINI

## MRADI WA KUONGEZA THAMANI KATIKA MILIMA YA TAO LA MASHARIKI (AVA)

Funded by the European Union

Adding Value to the Arc: Forests and Livelihoods in the South Nguru Mountains

Tanzania Forest Conservation Group
Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania

MTANDAO WA JAMII WA USIMAMIZI WA MISITU TANZANIA • MJUMITA •

# YALIYOMO


KUHUSU MRADI WA AVA ........ v
Mradi huu unatekelezwa na TFCG, MJUMITA, TFS na MVDC: ........ v

**UTANGULIZI ........ vi**
Kuhusu kitini hiki ........ vi

**SEHEMU YA KWANZA ........ 1**
1. SIFA ZA KUKU WA ASILI, FAIDA NA CHANGAMOTO ZAKE ........ 1
1.1 Sifa za Kuku wa Asili: ........ 1
1.2 Faida za Ufugaji wa Kuku wa Asili: ........ 1
1.3 Mapungufu ya Kuku wa Asili ........ 2
1.4 Changamoto katika ufugaji kuku wa asili ........ 2

**SEHEMU YA PILI ........ 3**
2.0 MIFUMO YA UFUGAJI KUKU ........ 3
2.1 Kufuga huria ........ 3
2.2 Kufuga nusu ndani – nusu nje ........ 3
2.3 Kufuga ndani ya Banda tu ........ 4

**SEHEMU YA TATU ........ 5**
3.0 BANDA LA KUKU ........ 5
3.1 Sifa za banda bora la Kuku ........ 5
3.2 Vifaa vinavyohitajika katika banda la kuku ........ 5
a) Vyombo vya Chakula: ........ 6
b) Vyombo Vya Maji: ........ 6
c) Viota: ........ 6
d) Vichanja vya Kupumzikia na Kulala: ........ 7

**SEHEMU YA NNE ........ 8**
4.0 UTUNZAJI WA KUKU WA ASILI ........ 8
4.1 Kuchagua kuku bora jike wa asili wa kufuga. ........ 8
4.2 Kuchagua jogoo bora wa mbegu ........ 8
4.3 Mayai kwa ajili ya kutotoa vifaranga. ........ 8
4.4 Kuwafanya kuku wengi kutotoa kwa wakati mmoja ........ 9

**SEHEMU YA TANO ........ 10**
5.0 ULEAJI WA VIFARANGA ........ 10
i. Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili: ........ 10
i. Uleaji wa vifaranga mfumo wa kubuni: ........ 10

Ufuatiliaji wa vifaranga ........ 11

**SEHEMU YA SITA** .......... **12**
6.0 UTENGENEZAJI CHAKULA CHA KUKU .......... 12

**SEHEMU YA SABA** .......... **14**
7.0 MAGONJWA YA KUKU .......... 14
Jinsi ya kuzuia magonjwa (kanuni) .......... 14

**SEHEMU YA NANE** .......... **17**
8.0 TIBA ZA ASILI ZA KUKU. .......... 17
Baadhi ya mimea inayotibu maradhi ya kuku: .......... 17

**SEHEMU YA TISA** .......... **1**9
9.0 KUWEKA KUMBUKUMBU ZA UFUGAJI .......... 19

**SEHEMU YA KUMI** .......... **1**9
10. MASOKO .......... 21
Marejeo .......... 22

# KUHUSU MRADI WA AVA

Lengo kuu la mradi ni kupunguza umasikini na kuboresha shughuli za kiuchumi kwa jamii zinazoishi kandokando ya misitu na zinazotegemea rasilimali zinazotokana na misitu. Mradi unatekelezwa kwenye Milima ya Nguru Kusini ambao ni chanzo muhimu cha bonde la Wami linalosambaza maji kwenye mji mdogo wa Madizini, Chalinze na miji ya Morogoro na jiji la Dar es Salaam. Eneo hili ni moja ya maeneo muhimu sana duniani kwa kuwa na wanyama na mimea ya kipekee na adimu iliyoko kwenye hatari ya kutoweka duniani. Kutokana na kuongezeka kwa utegemezi wa misitu ya Milima ya Nguru Kusini hali hii inatishia kuzorotesha shughuli za jamii na matokeo yake kupelekea kupotea kwa bioanuwai na makazi ya viumbe mbalimbali wanaoishi kwenye misitu hii.

Mradi unafadhiliwa na Umoja wa Nchi za Ulaya kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2013 hadi 2017.


## Mradi huu unatekelezwa na TFCG, MJUMITA, TFS na MVDC:

Tanzania Forest Conservation Group (Shirika la Kuhifadhi Misitu ya Asili Tanzania):
tfcg@tfcg.or.tz www.tfcg.org/nguru

MJUMITA (Mtandao wa Jamii wa Usimamizi wa Misitu Tanzania):
mjumitaorgorg@mjumita.org www.mjumita.org

Tanzania Forest Service (Wakala wa huduma za Misitu Tanzania):
mpingo@tfs.go.tz www.tfs.go.tz

Halmashauri ya Wilaya ya Mvomero:
dedmvomero@yahoo.com



# UTANGULIZI

## Kuhusu kitini hiki

Moja ya Matokeo/matarajio makuu ya utekelezaji wa Mradi wa AVA ni Kusaidia jamii kuibua miradi ya maendeleo ambayo ni rafiki wa misitu na mazingira., Hivyo moja -wapo ya miradi iliyoibuliwa na wanakijiji wakati wa zoezi la uibuaji miradi lililoendeshwa na wataalamu wa mradi na wa Halmashauri ya Mvomero ni ufugaji wa kuku wa asili. Mradi kwa kuona hitaji hili na fursa iliyopo ya kujiongezea kipato, hasa kwa kaya masikini, ulifanya zoezi la kutambua kaya maskini ambazo zinahitaji kupata mafunzo ya ufugaji wa kuku wa Asili. Vijiji 14 vilivyopo kwenye eneo la mradi vilifanya zoezi la kuainisha wakulima wanaohitaji elimu ya ufugaji wa kuku na ambao wako tayari kuanza mradi huu kwa kutumia rasilimali zao wenye na kwamba jukumu pekee la mradi ni kuwapa elimu na kufuatilitia utekelezaji wake. Baada ya kutambua mahitaji ya wakulima, mradi ulianza zoezi la kufundisha wakulima juu ya ufugaji wa kuku wa Asili kwa kutumia wataalam wa kata wa mifugo wenye uzoefu wa siku nyingi na wanaowatambua vizuri wafugaji walioko kwenye eneo la mradi . Baada ya mafunzo wanakijiji walionyesha kuwa na uhitaji wa kitini kwa ajili ya kujikumbusha mada mbalimabali zilizoendeshwa kwenye zoezi zima. Kwahiyo basi, kitini hiki kimekusanya maelezo kutoka kwenye majarida, vitabu mbalimbali na uzoefu wa wataalam wa mifugo ngazi ya kata ili kuweza kukidhi mahitaji ya wafugaji wa kuku wa Asili kwenye eneo la mradi. Mradi unaamini kitini hiki kitawasaidia wakulima, walimu na wanafunzi kuboresha ufugaji wa kuku wa Asili na hivyo kuinua pato la kaya.

# SEHEMU YA 1

## 1. SIFA ZA KUKU WA ASILI, FAIDA NA CHANGAMOTO ZAKE.

### 1.1 Sifa za Kuku wa Asili:

- Wastahimilivu wa magonjwa, lakini ni muhimu wakikingwa na baadhi ya magonjwa ya kuku kama mdondo, ndui ya kuku n.k. ili kuweza kuwaendeleza.
- Wana uwezo wa kujitafutia chakula ardhini, lakini ili kuwaendeleza ni lazima kuwapa chakula bora cha ziada.
- Wana uwezo wa kuatamia mayai, kutotoa, kulea vifaranga na ustahimilivu wa mazingira magumu (ukame, baridi nk).
- Nyama na mayai yake vina ladha nzuri kuliko kuku wa kisasa hivyo vina bei kubwa.
- Kwa kiasi fulani wana uwezo wa kujilinda na maadui kama vile mwewe.

### 1.2 Faida za Ufugaji wa Kuku wa Asili:

- Chakula – nyama ya kuku na mayai hutumika kama chakula muhimu cha wanadamu, chenye protini.
- Chanzo cha kipato – mkulima hupata fedha akiuza kuku au mayai.
- Chanzo cha ajira – ufugaji wa kuku hutoa ajira kwa jamii.
- Kuku hutumika kwenye shughuli za ndoa kama vile kutoa mahari na pia ni kitoweo muhimu katika sherehe hizo.
- Gharama nafuu za kuanzisha na kuendesha mradi huu.
- Ni kitoweo rahisi na chepesi kwa wageni kuliko wanyama wakubwa kama ng'ombe au mbuzi.
- Ni kitoweo kisichohitaji hifadhi, hutumika mlo mmoja au miwili na kumalizika.
- Kuku na mayai hutumika kwa tiba za asili.
- Jogoo hutumika kama saa anapowika nyakati za alfajiri na majira mengine ya siku.
- Hutuhabarisha iwapo kiumbe kigeni au cha hatari kwa mlio maalum wa kuashiria hatari.
- Mbolea – kinyesi cha kuku kinaweza kutumika katika kurutubisha mashamba ya mazao na mabwawa ya samaki.
- Kuendeleza kizazi cha kuku wa asili hapa nchini.
- Soko lipo la uhakika, ukilinganisha na kuku wa kisasa kwani nyama na mayai yake hupendwa zaidi na walaji.
- Manyoya ya kuku hutumika kama mapambo, pia huweza kutumiaka kutengenezea mito ya kulalia na kukalia.
- Shughuli za utafiti – kuku wanatumika katika tafiti nyingi za baiolojia, kama kutambua mambo ya lishe.
- Shughuli za viwandani:
- Mayai yenye mbegu ya jogoo hutumika katika kutengeneza dawa za chanjo.
- Magamba ya mayai yanaweza kutumika katika utengenezaji wa vyakula vya wanyama.
- Kiini cha njano cha mayai kinaweza kutumika kutengeneza mafuta ya kuoshea nywele *(shampoo).*

**1.3 ..........................................................................................................................................**
**Mapungufu ya Kuku wa Asili**

- Hutaga mayai madogo wastani wa gramu 47 ambapo kuku wa kisasa wastani wa gramu 55, aidha hutaga mayai machache wastani wa mayai 60 kwa mwaka ambapo kuku wa kisasa huweza kutaga hadi mayai 300 kwa mwaka.
- Ukuaji taratibu – kuku wa asili hukua taratibu kutokana na lishe duni. Kutokana na hali hiyo kuku huchukua muda mrefu (miezi sita) kufikia uzito wa kuchinjwa (kilo 1 - 1.5). Hali hii pia hufanya faida ya ufugaji wa kuku wa asili kuchukua muda mrefu kupatikana.
- Nyama yake ni ngumu (huchukua muda mrefu kuiva) ikilinganishwa na kuku wa kisasa.

### 1.4 Changamoto katika ufugaji kuku wa asili

- Mabanda: Ukosefu wa mabanda bora.
- Wezi, wanyama na ndege hushambulia kuku.
- Magonjwa: kama mdondo na ndui huathiri ufugaji wa kuku.
- Tabia na miiko ya baadhi ya jamii. Baadhi ya jamii za makabila hapa nchini huona ufugaji wa kuku kama ni kitu duni.
- Upatikanaji haba wa chanjo za magonjwa kama vile, mdondo, ndui, homa ya matumbo.


# SEHEMU YA 2

## 2.0 MIFUMO YA UFUGAJI KUKU

Ipo mifumo mitatu ya ufugaji wa kuku wa asili inayotumika nchini Tanzania. Mifumo hiyo ni Ufugaji huria, Ufugaji wa nusu huria na ufugaji wa ndani. Kila mfumo una faida na hasara zake. Mambo yanayomfanya mfugaji kuamua atumie njia fulani ya kufuga ni pamoja na uwezo wa kugharamia shughuli ya ufugaji wa kuku na ukubwa wa eneo alilonalo la kufugia. Katika sehemu hii utajifunza njia bora ya kufuga na utafanya maamuzi sahihi.

### *2.1 Kufuga huria*

Kuku huachwa wenyewe kujitafutia chakula na maji. Njia hii inatumika zaidi kufuga kuku wa kienyeji. Mara chache sana mfugaji huwapatia kuku chakula cha ziada. Kwa ufugaji huu lazima kuwe na eneo kubwa la kutosha kuku kuzunguka na kutafuta chakula. Kuku hulala eneo lisilo rasmi kama vile jikoni, kwenye kiambata n.k.



*Mfano wa Banda la Ufugaji Huria*

**Faida zake**
- Ni njia rahisi ya kufuga.
- Gharama yake pia ni ndogo.
- Kuku wanapata mazoezi ya kutosha.
- Kuku wanapata chakula mchanganyiko ambacho kinafaa kiafya.

**Hasara zake**
- Kuku huwa hatarini kuibiwa au kudhurika na wanyama wakali na hali mbaya ya hewa.
- Ukuaji wa kuku ni hafifu, hufikia uzito wa kilo 1.2 baada ya mwaka.
- Huharibu mazingira kama kula na mimea ya bustanini mazao kama nafaka.
- Ni rahisi kuambukizwa magonjwa.

### *2.2 Kufuga nusu ndani – nusu nje*

Huu ni mtindo wa kufuga ambapo kuku wanakuwa na banda lililounganishwana uzio kwa upande wa mbele. Hapa kuku wanaweza kushinda ndani ya banda au nje ya banda wakiwa ndani ya uzio.

Wakati wa mchana kuku huwa huru kushinda ndani ya banda hasa wanapotaka kutaga na wakati wa kuatamia au wanaweza kukaa ndani ya uzio nje.

**Faida za kufuga nusu ndani na nusu nje**

- Kuku wanakuwa salama mbali na maadui mbali mbali.
- Utaweza kuwalisha kuku wako vizuri hivyo wataweza kuongeza uzalishaji wa mayai na wa nyama (kwa kukua haraka).
- Itakuwa rahisi kwako kudhibiti wadudu na vimelea vinavyoweza kuleta magonjwa kwa kuku wako.
- Ni rahisi kuwatenganisha kuku katika makundi tofauti na kuwahudumia ipasavyo.
- Ni rahisi kutambua kuku wagonjwa kuliko kufuga huria.
- Kuku watapata mwanga wa jua wa kutosha pamoja na hewa safi.Wakati wa jua kali watakuwa huru kuingia ndani ya banda na kukaa kivulini.
- Kuku hawatafanya huharibifu wa mazao yako shambani au bustanini na kwa majirani zako.
- Utapata urahisi wa kukusanya na kupeleka mbolea bustanini au shambani. Changamoto ya kufuga nusu ndani na nusu nje.
- Huna budi uwe na muda wa kutosha kwa ajili ya kuwahudumia kuku wako.
- Pia utahitaji kuwa na eneo kubwa kiasi la kufugia.
- Pia utaingia gharama ya ziada kidogo ya kutengeneza banda na wigo na kuwapatia uku chakula cha ziada.
- Hata hivyo gharama za muda huo na za vifaa vingine zitafidiwa na mapato ya ziada utakayopata kwa kufuga kwa njia hii.

### *2.3 Kufuga ndani ya Banda tu*

Njia nyingine ni kuwafuga kuku ndani tu.
Katika njia hii, kuku hukaa ndani wakati wote. Njia hii ya ufugaji utumiwa zaidi na wafugaji wa kuku wa kisasa. Lakini yaweza kutumika hata kwa kuku wa asili hasa katika sehemu zenye ufinyu wa maeneo.

**Changamoto za ufugaji wa ndani ya banda tu**

- Unatakiwa uwe na muda wa kutosha wa kuwahudumia kuku wako kikamilifu.
- Pia unatakiwa kuwa na mtaji mkubwa wa kujenga banda na kuwanunulia kuku chakula.
- Ugonjwa ukiingia na rahisi kuambukizana.Vilevile kuku huweza kuanza tabia mbaya kama kudonoana, n.k.

**Faida za kufuga ndani tu**

- Ni rahisi kutambua na kudhibiti magonjwa.
- Ni rahisi kudhibiti upotevu wa kuku, mayai na vifaranga.
- Ni rahisi kuwapatia chakula kulingana na mahitaji ya kila kundi.
- Ni rahisi kuwatambua na kuwaondoa kuku wasiozalisha katika kundi.

Ni ufugaji upi unafaa zaidi kutumika kwenye mazingira ya vijijini?
Kwa ujumla, njia rahisi na inayopendekezwa kutumiwa na mfugaji wa kawaida kijijini ni ya ufugaji wa nusu ndani na nusu nje, yaani nusu huria. Hii inatokana na faida zake kama zilizoainishwa hapo awali. Kwa kutumia mfumo huu wa ufugaji, utaepuka hasara za kufuga kwa mtindo wa huria kama zilivyainishwa mwanzoni mwa sehemu hii ya kitabu hiki. Pia ukitumia mtindo wa ufugaji wa nusu huria utafanya ufugaji wako kwa njia bora zaidi ndani ya uwezo ulionao, kwa sababu kwa sehemu kubwa utatumia malighafi inayopatikana katika eneo lako.

# SEHEMU YA 3

## 3.0 BANDA LA KUKU

Ni muhimu kuwajengea kuku banda bora ili wapate kujikinga na mvua, baridi, wezi na wanyama. Banda la kuku linaweza likajengwa kando kando au nyuma ya nyumba ya kuishi. Eneo linapojengwa banda la kuku pawe:

- Panafikika kwa urahisi.
- Pasituamishe maji.
- Pasiwe pa mwelekeo wa upepo mkali

### 3.1 Sifa za banda bora la Kuku

Ukiamua kufuga katika banda kwa njia mbili zilizoelezwa awali utatakiwa kujenga banda lenye sifa zitakazokidhi mahitaji ya msingi ya kuku. Banda bora la kuku linatakiwa kuwa kama ifuatavyo:

Liwe jengo imara


- Pasiwe na sehemu zilizo wazi kwenye msingi na kati ya ukuta na paa.
- Banda lijengwe na vifaa vinavyopatikana katika mazingira yako ili liwe na gharama utakayoweza kumudu.
- Unaweza kutumia matofali ya udongo, udongo, miti, fito,n.k. Ukitumia fito au mabanzi ondoa maganda ili kuthibiti mchwa.
- Jengo imara litazuia maadui kama panya, vicheche, paka, nyoka na wezi kuingia ndani ya banda na kuwadhuru au kuwaiba kuku. Liwe rahisi kusafisha
- Kuta na sakafu visiribwe zisiwe na nyufa ili kurahisisha kusafisha.
- Pia itadhibiti kusiwe na wadudu wa kujificha katika nyufa kama papasi, viroboto n.k.
- Sakafu ya banda lazima iwekewe matandazo kama pumba ya mpunga au maranda ya mbao au mabaki ya mazao au nyasi kavu kutegemeana na kinachopatikana kwa urahisi katika mazingira yako.
- Matandazo haya husaidia kunyonya unyevu unaotokana na kinyesi cha kuku au maji yanayomwagika katika banda.
- Banda hubakia kavu bila kuwa na harufu mbaya na wadudu kama inzi hata vimelea vya magonjwa hudhibitiwa. Eneo la nje kuzunguka banda kuwe na usafi wa kudumu Hali ya usafi nje ya banda itafanya wadudu kama siafu au mchwa na wanyama kama panya na paka mwitu wakose maficho. Nje ya banda ndani ya uzio kuwe na miti midogo na mimea mingine midogo kwa ajili ya kivuli. Liwe na ukubwa (nafasi) unaolingana na idadi ya wastani wa kuku 10-15 kwa mita moja mraba kwa kuku wanaofugwa huria, ili wawe na nafasi ya kulala tu wakati wa usiku. Ila kwa kuku wanaofugwa kwa mfumo wa nusu ndani nusu nje wanastahili eneo la mita moja mraba kwakuku 4 - 5 ili kuruhusu nafasi ya vyombo vya chakula na maji.

### 3.2 Vifaa vinavyohitajika katika banda la kuku

Ufugaji wenye tija unahitaji kuhakikisha kuwa vifaa muhimu vinakuwemo ndani ya banda kwa uwiano unaotakiwa kati ya kuku na vifaa hivyo. Vifaa hivyo ni pamoja na:

i. Vyombo vya Chakula
ii. Vyombo vya Maji

iii. Viota
iv. Vichanja, na
v. Matandiko




a) **Vyombo vya Chakula:**

- Ni muhimu kuwa na vyombo vya kutosha ili kuwawezesha kuku kula pasipo kusongamana.
- Vyombo hivyo lazima viwe safi na bora ili kuongeza ufanisi katika kufuga kuku.



- Vyombo vinavyotakiwa ni vile vinavyoweza kuzuia upotevu wa chakula. Kuku wasipewe nafasi ya kuchakura ndani ya vyombo hivyo ili kupunguza kupotea kwa chakula. Unaweza kuzuia upotevu huo kwa kuweka vyombo hivyo juu ya mawe, gogo au kuvining'iniza.

- Vyombo vya chakula vinaweza kutengenezwa na mfugaji mwenyewe kwa kutumia vifaa mbalimbali vilivyomo katika mazingira yake na si lazima vile vilivyotengenezwa viwandani. Baadhi ya vitu vinavyoweza kutumika ni pamoja na kipande cha gurudumu la gari lililotumika, gogo lililochimbwa kati na kadhalika.




b) **Vyombo Vya Maji:**

Vyombo vya maji ni muhimu sana kwa kuku pasipo kuangalia wanafugwa kwa mtindo gani. Maji safi ni muhimu sana kwa kuku kwani huwafanya kuku kuwa na afya bora na kuongeza ufanisi katika utagaji wa mayai. Ni vyema kutumia vyombo vya maji ambavyo ni rahisi kuvifanyia usafi,visivyo na uwezekano wa kumwaga maji hovyo.

Vyombo vya maji ni vyema vikaning'inizwa ili kuwawezesha kuku kunywa maji kwa urahisi na pia kuzuia maji kuchafuliwa na kumwagwa kwa urahisi.

**c) Viota:**

Ni vyema kuwepo na sehemu maalumu ya kutagia ndani ya banda la kuku. Sehemu hii inatakiwa kuwa tulivu, faragha na yenye mwanga hafifu.

Kutokuwepo kwa viota husababisha kuku kutaga mayai hovyo na kupotea kwa mayai mengi pasipo kujua na uanguaji huwa mbaya, hivyo kupunguza uzalishaji wa kuku na kurudisha nyuma shughuli ya uzalishaji.


Kiota kinatakiwa kuwa na nafasi nzuri ya kumuwezesha kuku kuenea na kuweza kujigeuza. Kwa wastani kiota kinatakiwa kuwa na urefu wa sentimita 35, upana wa sentimita 35 na kina cha sentimita 35.





Pia kiota kiwekwe juu kwa sentimita 50 toka sakafuni ili kumfanya kuku kujisikia salama zaidi. Viota vinatakiwa viandaliwe mapema kulingana na idadi ya makoo uliyo nayo. Ndani ya kila kiota utatakiwa kuweka matandiko ili kuongeza joto na usalama wa mayai. Idadi ya viota iwe robo tatu yaidadi ya kuku waliofikia umri wa kutaga.

d) **Vichanja vya Kupumzikia na Kulala:**




Kwa asili kuku hupendelea zaidi kulala juu kama kwenye miti kwani hujisikia kuwa na usalama zaidi kuliko wakiwa katika sehemu isiyo na mahali pa kudanda. Hivyo ili kuwafanya kuku wajisikie vizuri hapana budi kuwatengenezea vichanja sehemu ya nje wanaposhinda na kula chakula, na pia ndani ya banda ili kuwawezesha kulala vizuri nyakati za usiku.Kwa kawaida vichanja vinatakiwa vitengenezwe kwa urefu wa mita moja toka ardhini. Vijiti vya juu vyapaswa kuwa vya duara vyenye kipenyo kinachowezesha miguu ya kuku kuzunguka vizuri na kubana.



**Faida za kutumia vichanja:**

Huzuia kuku kulala hovyo ndani ya viota.

Hupunguza mashambulizi ya wadudu kama viroboto, utitiri na wadudu wengineo wanaoweza kuwa kwenye matandiko.

**Uwekaji wa Matandiko:**

Matandiko yanaweza kuwa ni maranda ya mbao, makapi ya mpunga na kahawa n.k. Matandiko husaidia sana kufyonza unyevunyevu toka ardhini na kutoka kwenye kinyesi. Pia huzuia maradhi yatokanayo na baridi na unyevunyevu hususani kwa vifaranga. Utahitaji matandiko yenye ujazo wa unene wa sentimeta 5 hadi 10 ili kuwawezesha kuku wako kuwa katika hali iliyo nzuri. Maraunapoona dalili za matandiko kulowa inabidi kuyaondoa mara moja kwani ni rahisi kuoza na kuleta madhara kwa kuku.

Inashauriwa kubadili matandiko ndani ya banda la kuku kila inapobidi.

# SEHEMU YA 4

## 4.0 UTUNZAJI WA KUKU WA ASILI

### 4.1 Kuchagua kuku bora jike wa asili wa kufuga.

Aina za kuku wa asili wanaopatikana hapa nchini ni pamoja na Kuchi (Kuza), Poni (Kishingo), Njachama, Kinyavu, Mbuni na Tongwe (Msumbiji). Mfugaji anaweza kuongeza uzalishaji kwa kuchagua kuku mwenye sifa zifuatazo:-

- ✓ Uwezo wa kutaga mayai mengi (kati ya 15-20) katika mzunguko mmoja wa utagaji
- ✓ Uwezo wa kuatamia na kuangua vifaranga wengi,
- ✓ Uwezo wa kustahimili magonjwa,
- ✓ Anayetoka maeneo yasiyo na magonjwa; na
- ✓ Umbo kubwa na kukua haraka.



### 4.2 Kuchagua jogoo bora wa mbegu.

Jogoo wa mbegu anatakiwa awe na sifa zifuatazo:

- ✓ Achaguliwe kutoka kwenye koo zenye sifa ya kutaga mayai mengi,
- ✓ Mrefu, umbo kubwa, miguu imara na yenye nguvu,
- ✓ Awe ukiko mzuri na usioangukia upande mmoja,
- ✓ Awe machachari, ushawishi kwa mitetea na ari ya kupanda; na
- ✓ Uwezo wa kupanda akiwa na umri wa miezi 7 – 10
- ✓ Jogoo mmoja mwenye sifa hizi anweza kupanda mitetea kumi.

### 4.3 Mayai kwa ajili ya kutotoa vifaranga.

Uchaguzi wa Mayai Mayai kwa ajili ya kutotoa vifaranga yawe na sifa zifuatazo:-

- ✓ Yaliyorutubishwa na jogoo,
- ✓ Yasiwe na nyufa,
- ✓ Yasiwe na maganda tepetepe,
- ✓ Yasiwe na kiini kilichovunjika,
- ✓ Yawe na ukubwa wa wastani; na
- ✓ Yasiwe yamekaa zaidi ya wiki mbili baada ya kutagwa.

Wastani wa jogoo mmoja kwa majike kumi (10).

### Kuchagua mayai ya kuanguliwa

Mayai yanayofaa kuanguliwa yawe na ukubwa wa wastani, yasiwe na nyufa, yasiwe ya mviringo kama mpira, yasiwe na uchafu, mayai mazuri ni yale yaliyotagwa na kuku aliyepandwa na jogoo.

### Uanguaji wa vifaranga wa asili

Kwa kawaida kuku mmoja anaweza kuatamia mayai 12 hadi 15 kwa mara moja, kuku awekewe mayai ya kuatamia wakati wa kuatamia unapofika.Inashauriwa kumwekea kuku mayai ya kuatamia wakati wa usiku kwani akiwekewa mchana anaweza kuyaacha.

**Kutayarisha kuku wa kuatamia**

kuku wanaotazamiwa kuatamia lazima wachaguliwe kwa makini siku mbili kabla ya kuatamia ili kuhakikisha kwamba hawana chawa, utititri au viroboto. Kuwepo kwa wadudu hao husababisha kuku wasitulie kwani huwakosesha raha hali hii husababisha kuanguliwa kwa vifaranga vichache.

**4.4 Kuwafanya kuku wengi kutotoa kwa wakati mmoja**

Kuna uwezekano mkubwa tu wa kuweza kuwandaa kuku na kuweza kutotoa kwa siku moja. Njiani rahisi na inaweza kuongeza tija katika ufugaji wa kuku wa Asili. Ili uweze kutotolesha kuku kwa wakati mmoja fanya yafuatayo:

- ✓ Kuku anapotaga kila siku weka alama kila yai linalotagwa aidha namba au tarehe kulingana na siku aliyotaga.
- ✓ Yanapofika mayai matatu yaondoe na muwekee mayai bandia na huku ukiendelea kukusanya na kuweka alama mayai yanayoendelea kutagwa kila siku.
- ✓ Mara kuku anapoanza kuatamia unaweza kumuongezea mayai bandia na kufikia 8 hadi10.
- ✓ Fanya hivyo kwa kila kuku anayetaga hadi utakapopata idadi inayoweza kukupatia vifaranga wengi kwa wakati mmoja.
- ✓ Chagua mayai ya kuatamia ukianza na yai la mwisho kutagwa. Wawekee kuku wote mayai siku moja kwa kuondoa mayai bandia na kuwawekea mayai ya kweli wakati wa usiku.
- ✓ Kuku huendelea kuatamia mpaka vifaranga vitoke hivyo ukimwekea mayai yasiyo na mbegu, atakaa hapo hapo kwa muda mrefu. Kwa kawaida kuku huatamia mayai kwa muda wa siku 21kabla ya vifaranga kuanguliwa.

***Muhimu:*** *Inashauriwa kutokuwa na majogoo wengi, hivyo yakupasa kudhibiti ongezeko la majogoo ndani ya banda. Waweza kufanya hivyo kwa kuhakikisha unayatambua mayai yanayoweza kuwa na mbegu ya jogoo mapema. Utafiti unaonyesha kuwa mayai membamba yenye ncha kali huwa na mbegu ya jogoo, hivyo yanaweza kuondolewa na kuliwa na familia au kuuzwa. Kwa utaratibu huo utakuwa umedhibiti ongezeko la majogoo ndani ya banda, isipokuwa kama unahitaji majogoo kwa ajii ya biashara waweza kuzalisha mengi zaidi.*

# SEHEMU YA 5

## 5.0 ULEAJI WA VIFARANGA

Vifaranga ni hatua ya mwanzo ya ukuaji wa kuku, hivyo ni bora kuchukua tahadhari ili kuhakikisha ukuaji ulio bora wa vifaranga hao. Vifaranga vinahitaji malezi makini kuepusha magonjwa yanayoweza kusababisha vifo na hivyo kupunguza idadi ya kuku unaotarajia kuwa nao. Uhakika wa kuwa na kuku walio bora na wengi utategemea matunzo bora ya vifaranga utakayotoa tangu siku ya kwanza vifaranga vitotolewe. Vifo vingi vya vifaranga hutokea siku za mwanzoni vikishatotolewa. Hivyo basi, ili mfugaji aweze kupata tija na mafanikio kwa haraka kutokana na ufugaji wa kuku wa Asili, ni vyema kuhakikisha vifaranga vinalelewa katika mazingira mazuri toka siku ya kwanza.




Vifaranga huhitaji joto la ziada katika kipindi cha mwanzo cha ukuaji ambacho ni kati ya siku 1 hadi wiki ya nane. Hapa nchini, mara nyingi njia ya asili ya kutumia kuku wazazi hutumika kutoa joto la ziada kwa vifaranga kwa kipindi cha wastani wa siku 90.

Kuna mifumo (2) miwili ya uleaji wa vifaranga ambayo ni:

i. Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili.
ii. Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa kubuni.

**i. Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili:**

Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa asili ni ule uliozoeleka, ambapo kuku mwenyewe baada ya kutotoa hutembea na vifaranga vyake akivisaidia kutafuta chakula na kuvikumbatia kila baada ya muda fulani ili kuvipatia joto. Mfumo wa asili umekuwa hauna tija kwa kusababisha ukuaji wa vifaranga kuwa duni na vingi kushambuliwa na wanyama na ndege na vingine kufa. Na vile vile mizunguko ya utagaji wa kuku kwa mwaka huwa michache. Kwa kutumia mfumo huu vifaranga hulelewa kwa takribani miezi (3) mitatu.Kama utalea vifaranga kwa mfumo wa asili, basi ni vizuri kumtenga kuku mwenye vifaranga na kumuweka kwenye chumba cha pekee ili vifaranga visishambuliwe na kuku wengine hali kadhalika kuwalinda na wanyama na ndege wanaoshambulia vifaranga kama vile vicheche, mwewe na kunguru.

**ii. Uleaji wa vifaranga mfumo wa kubuni:**

Uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa kubuni ulikuwa unatumika zaidi kwa ufugaji kuku wa kisasa ambao hutotolewa kwa wingi sana, ambapo vifaranga huwekwa kwa pamoja kwenye chumba maalum na kupatiwa joto maalum, chakula pamoja na maji. Utaratibu huu pia unaweza kutumika kwa kuku wa Asili kwani kitu muhimu ni joto la kutosheleza ukuaji.

Kwa kutumia mfumo wa kubuni, kuku wanaweza kunyang'anywa vifaranga vyao mara tu baadaya kutotoa na kuviweka kwenye Bruda na hao kuku wakaachwa bila vifaranga. Baada ya majuma mawili, kuku walionyang'anywa vifaranga hao huanza tena kutaga na kuendelea na uatamiaji hadi kutotoa tena. Kwa mfumo huu kuku anaweza kutotoa mara 5 hadi 6 badala ya mara 2 hadi 3 kwa mwaka kama ilivyo sasa.

**Kuna njia mbili za uleaji wa vifaranga kwa mfumo wa kubuni:**

i. **Njia ya uleaji wa vifaranga kwa kutumia nishati**

Utaratibu huu unahusu kutunza vifaranga kwenye mzingo (mduara) ndani ya chumba na kuvipatia joto kwa kutumia taa ya kandili (chemli), taa ya umeme au jiko la mkaa. Hata hivyo, njia hii ina gharama kubwa na wakati mwingine upatikanaji wake si wa uhakika. Kwa njia hii unaweza kupima joto katika mzingo kama linatosha au la kwa kuangalia hali ya usambaaji wa vifaranga ndani ya mzingo.

ii. **Njia ya uleaji wa vifaranga isiyotumia nishati**

Njia hii hutumika kulelea vifaranga bila ya msaada wa nishati ya kuongeza joto. Njia hii ni nzuri kwa wafugaji wadogo wadogo hasa waishio vijijini kwani hakuna gharama za kutafuta nishati ili kuwapatia joto badala yake joto la vifaranga wenyewe huwatunza na kuwapatia hifadhi maalum inayohitajika.

**Ufuatiliaji wa vifaranga**

Kuanzia wiki 1 – 4. Wiki ya kwanza

Siku ya kwanza hadi ya tano (1 – 7) vifaranga wapewe

- ✓ Chick formula (dawa ya vitamini ya vifaranga) kwenye maji kwa muda wa siku 5 Chakula cha vifaranga cha kuanzia.
- ✓ Chanjo ya mdondo angalau kati ya siku ya 5 hadi 7.
- ✓ Vifaranga wawekwe kwenye banda safi lililowekwa maranda (yasiwe mepesi yenye vumbi kwani yatawaletea vifaranga mafua.
- ✓ Vifaranga wakae na mama yao ili awapatie joto (kuwatamia) au wawekwe kwenye chumba maalumu chenye joto.

Siku ya 8 – 14

- ✓ Vifaranga waendelee na chakula cha vifaranga
- ✓ Siku ya 12 hadi 14 wapewe dawa ya kinga ya kuvaa makoti (kuhara damu)

Wiki ya tatu

Siku ya 15 – 21

- ✓ Chakula cha vifaranga kiendelee.
- ✓ Vifaranga warudie kupewa dawa/vitamin ya vifaranga (chick formula ) kwa muda wa siku tano
- ✓ Siku ya 20 – 21 wapewe dawa ya minyoo ya kuku. Dawa ya minyoo inatakiwa uwape kuku wote ulio nao bila ya kujali kundi. Baada ya miezi mitatu kuku wote wanatakiwa kupewa dawa ya minyoo tena.
- ✓ Banda la kuku (vifaranga) lifagiliwe na kuwekwa tena maranda safi.
- ✓ Kama uliwapa chanjo ya kuchanganya na maji inabidi urudie siku ya 25. WIKI YA NNE: Rudia dawa ya kuvaa makoti (Esb3).
- ✓ Vifaranga waendelee na chakula.
- ✓ Vifaranga wapewe dawa za kinga ya magonjwa mbalimbali kulingana na ushauri wa mtaalamu

Madawa hayo ni kama

- Antibiotic zilizochanganywa na vitamini *(OTC Plus*)
- Madawa aina ya salfa- *Trisulmycine, S-Dime, Fluquine*

# SEHEMU YA 6

### 6.0 UTENGENEZAJI CHAKULA CHA KUKU

Chakula cha kuku lazima kiwe na viini lishe muhimu kama vile:-

- ✓ Protein.
- ✓ Wanga.
- ✓ Madini.
- ✓ Vitamini.

Hakikisha chakula unachotengeneza kinakuwa na mchanganyiko wa vyakula vifuatavyo:

- ✓ Vyakula vya kujenga mwili kama vile ya kunde, samaki, mashudu ya ufuta, pamba na alizeti.
- ✓ Vyakula vya kulinda mwili na kukinga mwili usipate maradhi kama kabichi, michicha, majani ya mapapai na nyasi mbichi.
- ✓ Vyakula vinavyojenga mifupa kama vile aina ya madini, chokaa, mifupa iliyosagwa, chumvi. Ukosefu wa vitamini na madini kama kalisiamu na Fosforasi husababisha matege, kukunjamana kwa vidole, kufyatuka kwa misuli ya goti na kupofuka macho.

Mambo ya kuzingatia kabla ya kutengeneza chakula cha kuku

- ✓ Jinsi ya kupata vyakula vya aina mbalimbali
- ✓ Kiasi cha viini lishe vinavyohitajika kulingana na umri wa kuku kwa mfano] vifanga wanahitaji protein asilimia 18 hadi 22, kuku wanaokuwa wanahitaji asilimia 17 hadi 19, kuku wa mayai wanahitaji asilimia 15 hadi 17

Unaweza kuamua kuchanganya kilo 50 zaidi au chini ya hapo ya mchanganyiko huu kulingana na kiasi utakachohitaji kwa kugawanya kiasi cha uwiano kutokana na uwezo wako au idadi ya kuku unaowafuga.

**Jedwali 1: Mchanganyo wa chakula cha kuku cha kilo 50**

| **Na.** | **Aina ya chakula** | **Mchanganyiko (katika kilogramu) kwa ajili ya:** | | |
|---|---|---|---|---|
| | | **Vifaranga** | **Kuku wanao kua** | **Kuku wazazi** |
| 1 | Mahindi yalibarazwa | 8 | 8 | 8 |
| 2 | Pumba za Mahindi | 20 | 20 | 20 |
| 3 | Mashudu ya alizeti | 8 | 7 | 10 |
| 4 | Unga wa dagaa | 6 | 6 | 3.5 |
| 5 | Unga wa mifupa | 0.75 | 1.5 | 3 |
| 6 | Chokaa ya mifugo | 0.75 | 2 | 4 |
| 7 | Chumvi ya mezani | 0.5 | 0.5 | 0.5 |
| 8 | Soya iliyobarazwa | 3 | 3 | - |
| 9 | Unga wa damu | 1 | 1 | - |
| 10 | Premix | 1 | 1 | - |
| 11 | Egg booster | - | - | 1 |
| | **Jumla** | **50** | **50** | **50** |

**Baadhi ya vyakula vyenye asili zifuatazo pia vinafaa kulisha kuku:**

i. **Mizizi** - Mihogo, Viazi vitamu, Mbatata, Magimbi.

ii. **Nafaka** - Mahindi, Mpunga, Mtama, Ulezi, Pumba za nafaka zote.

iii. **Mboga** - Jamii ya mikunde, mboga za majani, nyanya, pilipili, majani laini ya ukoka, majani yamapapai, lukina, milonge na kisamvu.

iv. **Matunda** - kama vile Mapapai, Maembe na Matikiti maji.

v. **Mashudu** - Kama vile Karanga, Ufuta, Mashudu ya pamba, Alizeti, Soya, Machicha ya nazi.

vi. **Wadudu mbalimbali** - Panzi, Mchwa, Minyoo ya ardhini, Mende, Funza, Kumbikumbi n.k.

**Muhimu: Hakikisha kuku wanapata maji ya kunywa ya kutosha, ni vizuri kuku wanaofugwa huria wawekewe maji ya kunywa chini ya vivuli vya miti muda wote nyakati za mchana.**

SEHEMU YA 7

## 7.0 MAGONJWA YA KUKU

Magonjwa husababishwa na virusi, bacteria, vimelea, minyoo, viroboto, chawa, utitiri, lishe duni na uchafu.

Kuwatenga wagonjwa- kuku wagonjwa watengwe mbali na kuku wagonjwa ili ugonjwa usisambae kwa kuku wote Kuku huweza kushambuliwa na magonjwa mbalimbali ambayo husababisha hasara kubwa kubwa kwa mfugaji . hasara hiyo ni kama vile

- ✓ Gharama ya matibabu
- ✓ Kudumaa kwa kuku
- ✓ Vifo vya kuku
- ✓ Upungufu wa mayai

**Jinsi ya kuzuia magonjwa (kanuni)**
Usafi – ni muhimu sana kwa ajili ya kuzuia magonjwa
Chanjo- kuku wapatiwe chanjo dhidi ya ugonjwa wa kideri (Mdondo)
Kunywesha dawa za minyoo – kuku wapatiwe dawa za minyoo kila baada ya miezi mitatu

Magonjwa yanayosababishwa na virusi
Mdondo – new castle
Dalili za ugonjwa

- Kuku kukohoa Kuhema kwa shida
- Hutokwa na ute mdomoni na pua
- Hupatwa kizunguzungu
- Kuharisha mharo wa kijani na njano
- Hatimaye kuku hufa gafla
- Vifo huweza kufikia asilimia 90

Kinga na tiba

- Usafi wa banda na vyombo
- Usafi wa mazingira na kuchoma mizoga inayoweza kuletwa na ndege
- Usiruhusu watu kuingia kwenye banda ovyo
- Kuku wapewe kinga wakiwa na umri wa siku 5-7
- hakuna tiba dhidi ya ugonjwa huu

Ndui ya kuku

- kuku hupatwa na vipele vya mviringo kwenye upanga, masikio, miguu na sehemu zisizo na manyoya.
- Vifo vichache kwa kuku wa kubwa, wadogo hufa nusu ya kundi

Kinga na tiba

- Kuku wapewe chanjo wakiwa na umri wa miezi 2
- Wapewe vitamin na antibiotic
- Usafi wa banda na mazingira
- Hakuna tiba

Homa ya matumbo
Dalili
- Kuku huharisha mharo wa kijani
- Vilemba na upanga hupauka kutokana na upungufu wa damu
- Manyoya husimama
- Vifo huweza kufikia asilimia 50

Kinga na tiba
- Usafi wa banda
- Tibu kwa kutumia dawa zinazoshauriwa na wataalamu kama vile Esb3

Kipindupindu
Dalili
- Kuku huhara mharo wa njano
- Husinzia na kulegea
- Hulala kichwa kikining'inia kwenye mabawa
- Magoya husimama
- Hushindwa kusimama hatimaye hufa
- Vifo huweza kufikia asilimia 50
- Kinga na tiba  Usafi wa banda, vyombo na mazingira yake
- Tumia dawa ya chanjo kwa kufuata ushauri wa mtengenezaji wa chanjo  Ugonjwa huweza kutibika kwa dawa aina ya sulfa

Mafua ya kuku Coryza
Dalili
- Kuvimba uso na macho
- Kamasi hutiririka toka puani na mdomoni
- Hukohoa  Huhema kwa shida na kukoroma
- Mayai hupungua asilimia 10 – 40

Kinga na tiba
- Usafi wa banda na mazingira yake
- Kuku wagonjwa watengwe na ikibidi wachinjwe
- Wapewe dawa ya chanjo siku 2 kabla ya kuanzwa CTC 30%

Minyoo
Ni wa wadudu wanaoleta madhara kwa kuku na hata kwa wanyama wengine. Kuku hupata minyoo kwa kula vyakula vyenye kinyesi chenye wadudu.

Dalili
- Kuku hudumaa
- Manyoya huwa hafifu
- Damu hupungua
- Kupungua uzito na kukonda
- Utagaji wa mayai hupungua
- Minyoo huweza kuonekana kwenye kinyesi

Kinga
- Safisha banda kwa dawa ya kuuwa wadudu
- Badilisha matandazo
- Safisha vyombo vya chakula na maji

- Tenganisha kuku wakubwa na wadogo
- Kuku wapewe dawa za kuzuia minyoo kila baada ya miezi mitatu Kwa ushauri zaidi Muone mtaalamu wa mifugo.

**Kuhara damu *(Coccidiosis)***:
Ugonjwa huu husababishwa na vimelea aina ya *Protozoa* na hushambulia kuku wote wakubwa na wadogo ila huathiri zaidi kuku wadogo.

**Jinsi unavyoambukiza:**
- Kula chakula chenye kinyesi au maji yenye vimelea vya ugonjwa huu.

Dalili:
- Kuharisha kinyesi kilichochanganyika na damu
- Kuku kudhoofu na kupungua uzito.
- Kuku kuzubaa na kushusha mabawa kamakavaa koti.
- Kuku kujitenga na wengine.
- Kupoteza hamu ya kula.

Tiba:
- Dawa aina ya *Amprolium, Oxytetracycline* au Salfa ambayo huchanganywa kwenye maji na kupewa kuku kwa siku 5 hadi 7.

Kinga:
- Vifaranga wakifikia umri wa siku saba (7) wapewe *Amprolium* kwa siku tatu (3) mfululizo, hata kama dalili za ugonjwa hazijajitokeza.
- Tenganisha vifaranga na kuku wakubwa
- Kuku wagonjwa watengwe na kupewa tiba mara moja
- Zingatia usafi wa banda na vyombo vya chakula na maji

**Ukosefu wa Vitamini 'A':**
Ukosefu wa vitamini 'A' ni tatizo la lishe ambalo huwakabili kuku kutokana na ukosefu wa chakula chenye vitamini hii. Mara kwa mara hujitokeza baada ya kipindi kirefu cha kiangazi kwa ajili ya ukosefu wa majani mabichi.

Dalili za ukosefu wa vitamini 'A':
- Kuku kudumaa kutokana na kutokula vizuri.
- Macho huvimba na kutoa uchafu mzito kama sabuni iliyolowana.

Tiba:
- Hakuna tiba itakayomponyesha kuku baada ya dalili hizi kujitokeza na matokeo yake ni kifo.
- Hata hivyo kuku wote waliobakia katika banda lako wapewe dawa ya vitamini za kuku ambazo pia huwa na vitamini A kwani watakuwa na upungufu japokuwa dalili za ugonjwa hazijajitokeza.

Kinga:
- Hakikisha kuku wanapata majani ya kijani katika malisho yao. Walimie mchicha au wachumie majani mabichi kutoka sehemu zenye maji. Unaweza kuwapa vitamini za kuku za dukani kwa kufuata mapendekezo ya watengenezaji.

SEHEMU YA 8

## 8.0 TIBA ZA ASILI ZA KUKU.

Madawa ya asili yatokanayo na mimea yanayosaidia katika tiba na kinga za maradhi mbalimbali ya kuku.

Sehemu za mimea zinaweza kuwa: Majani, Magome, Mbegu, Maua au Matunda
Umuhimu wa kutumia tiba zenye asili ya mimea:

- Hupatikana kwa urahisi.
- Ni rahisi kutumia.
- Gharama nafuu.
- Zinatibu vizuri.
- Hazina madhara.

**Baadhi ya mimea inayotibu maradhi ya kuku:**
**Mwarobaini** (Majani, Mizizi, Magome): Hutibu magonjwa yafuatayo:

✓ Typhoid.
✓ Kuzuia Kideri.
✓ Kuhara.
✓ Mafua.
✓ Vidonda.

Shubiri Mwitu *(Aloe vera):*
Chukua majani 3-5 makubwa, katakata na loweka ndani ya maji lita 10 kwa masaa 12 hadi 16. Wape kuku kwa siku 5 - 7. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine baada ya masaa 12.

Mchanganyiko huu unaweza kutibu:

- Kideri/Mdondo (Mdonde/Chikwemba/Kitoga/Chinoya/Sotoka) inyweshwe kabla kwa kinga.
- Homa ya matumbo *(Typhoid).*
- Mafua *(Coryza).*
- Kipindupindu cha kuku *(Fowl Cholera).*

**Mtakalang'onyo** *(Euphorbia):*
Majani makubwa 3-5, ponda, weka katika lita 10 za maji kwa masaa 12-16, chuja na wape kuku. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine.

Mtakalang'onyo hutibu:

- Kideri/Mdondo (Mdonde/Chikwemba) - inyweshwe
- kabla kuzuia
- Gumboro.
- Ndui.
- Kuhara damu *(Coccidiosis).*

Mbarika (Nyonyo):

- Hutibu Uvimbe. Weka majani ya mbarika ndani ya majani ya mgomba kisha weka ndani ya jivu la moto, kisha kanda sehemu yenye uvimbe kwa kutumia majani hayo ya mbarika.

Mlonge *(Mlonje):*
Ina vitamini A na C. Chukua majani ujazo wa mikono miwili (gao mbili). Kisha yapondeponde na kuyaweka katika lita 10 za maji na iache kwa masaa 12-16, chuja na wape kuku. Isiyotumika mwaga na tengeneza nyingine.

Mlonge hutibu:
- Mafua.
- Kideri - inyweshwe kabla kwa kukinga
- Kipindupindu cha kuku *(Fowl Cholera).*

Ndulele *(Dungurusi, Makonde, Tura/Ndula):*
- Majani hutibu Minyoo.
- Matunda hutibu Vidonda.

Papai *(Majani):*
- Chemsha magao mawili ndani ya maji lita 6 hadi ubakie na lita 1. Poza kisha chuja.

Hutibu
- Minyoo

Mwembe:
Majani magao mawili, ponda na chemsha ndani ya lita 6 za maji hadi ibaki lita 1. Wape kwa siku moja.
Mwembe hutibu:
- Homa ya matumbo.
- Mafua.
- Kinga ya Kideri/Mdondo.

Mpira:
Chemsha majani au mizizi
Mpira hutibu:
- Tumbo
- Vidonda na majipu

Mpira:
Chemsha majani au mizizi. Mpira hutibu:
Tumbo
Vidonda na majipu

Minyaa *(Cactus):*
Hii ni aina yenye majani manene-hadi kufikia nusu nchi na mapana hadi kufikia upana wa viganja viwili vya mikono.
Minyaa hutibu: (Angalia inaunguza au kubabua).
- Vidonda.
- Ngozi.
- Uzazi.

Pilipili Kichaa:
Pondaponda kiasi kisha changanya na maji na wawekee kuku wawe wanakunywa kwa muda wao. Inasemekana inasaidia kutibu mdonde (lakini mapema kabla maradhi kuingia).

# SEHEMU YA 9

## 9.0 KUWEKA KUMBUKUMBU ZA UFUGAJI

Kumbukumbu za mradi wa kuku ni muhimu sana katika mazingira ya sasa ambayo kuku hufugwa kwa ajili ya biashara zaidi na sio kitoweo tu. Kumbukumbu hizi endapo zitatunzwa vizuri zitamwezesha mfugaji kusimamia mradi wake vizuri na kutambua kama shughuli zake za ufugaji zinafanyika kwa ufanisi mkubwa au la. Pia kumbukumbu hizi zitasaidia kuonesha yafutayo:

- Faida au hasara inayotokana na kuendesha shughuli za ufugaji.
- Mtindo na namna ya utendaji wa shughuli za ufugaji.
- Matukio muhimu yaliyotokea ndani ya mradi kama vile aina ya magonjwa yaliyoshambulia kuku na chanjo na tiba zilizotumika, kiwango cha utagaji wa mayai n.k.
- Kuonesha kwa undani namna ya shughuli ilivyoendeshwa muda uliopita au mbinu zilizotumika.
- Maendeleo ya kuku.
- Aina ya Magonjwa yaliyoshambulia kuku.
- Chanjo na tiba zilizofanyika.

**Faida za kumbukumbu:**
- Zinamuwezesha kugundua makosa na kuweka mpangilio wa masahihisho ya makosa
- Ni namna ya kuongeza na kuendeleza uwezo wa usimamizi na uongozi wa mfugaji.
- Huwezesha kufanya maamuzi sahihi yahusuyo mradi.

**Kumbukumbu zimegawanyika katika sehemu zifuatazo:**
- Kumbukumbu za uzalishaji.
- Kumbukumbu za fedha.
- Kumbukumbu za rasilimali zote katika uzalishaji.
- Kumbukumbu za matibabu na kinga

1. **Kumbukumbu za uzalishaji:**

Hizi zitamwezesha mfugaji kujua kiasi cha mayai yanayotagwa na vifaranga waliotototolewa pia kujua idadi ya kuku wanaokufa kwenye banda lake hivyo aweze kuchukua tahadhari.

2. **Kumbukumbu za fedha, matumizi na mapato:**

Hizi zitamsaidia mfugaji kujua uwiano wa mapato na matumizi ili aweze kujua kama anapata faida au hasara ya mradi wa ufugaji wa kuku.

**Jedwali 2: Mfano wa kumbukumbu (Idadi ya kuku)**

| Mwezi | | | | | Mwaka | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Tarehe | Idadi ya kuku | | | | Vifo/Mauzo | Baki | Maelezo |
| | Mitetea | Majogoo | Vifaranga | Jumla | | | |
| 1 | | | | | | | |
| 2 | | | | | | | |
| 3 | | | | | | | |
| 4 | | | | | | | |
| 5 | | | | | | | |

**Jedwali 3 Kumbukumbu ya Uatamiaji na Utotoaji**

| Tarehe/mwezi | Idadi ya mayai | | | Maelezo |
|---|---|---|---|---|
| | Yaliyoatamiwa | Yaliyoanguliwa | Yasioanguliwa | |
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| Jumla | | | | |

**Jedwali 4: Kalenda ya Chanjo/Tiba**

| Ugonjwa | Miezi | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 |
| Kideri | | | | | | | | | | | | |
| Ndui | | | | | | | | | | | | |
| Gumboro | | | | | | | | | | | | |

**Jedwali 5: Mapato na Matumizi:**

| Matumizi | | | Mapato | |
|---|---|---|---|---|
| Tarehe/Mwezi | Shughuli | Kiasi cha fedha shughuli | Chanzo | Kiasi cha fedha |
| 1 | | | | |
| 2 | | | | |
| 3 | | | | |
| 4 | | | | |
| 5 | | | | |
| Jumla | | | | |

# SEHEMU YA 10

## 10. MASOKO

Katika biashara ya aina yoyote mzalishaji hana budi afahamu mambo kadhaa ya msingi yatakayomsaidia kufanya maamuzi ya kumuwezesha kupata faida ya juu katika biashara anayoifanya:




Kwanza kabisa ajiulize kama bidhaa anayozalisha ina soko? Na kama soko lipo:

- Lipo wapi na hali ya miundombinu za kulifikia iko vipi ( ili afahamu gharama ya kufika sokoni kama utaamua kuuzia sokoni).
- Bidhaa inahitajika kwa wingi kiasi gani na wakati gani sokoni
- Soko linahitaji bidhaa yenye sifa zipi ( ubora n.k. ili uzalishe sawa na matakwa ya soko n.k)
- Kama wanunuzi watakuwa na utayari kununulia unakozalishia, je unao uwezo wa kutosheleza mahitaji yao (ili uweze kujipanga kukidhi mahitaji kwa kuongeza uzalishaji au kwa kuungana na wazalishaji wengine).
- Linganisha bei ya bidhaa sokoni na bei ya kuuzia unakozalishia (ili ujue palipo na faida zaidi kwako baada ya kuondoa gharama za kufuata soko) Ila ukiamua kuuzia sokoni hakikisha unao uwezo wa kushindana na wauzaji wengine huko sokoni. Majibu ya maswali haya ndiyo yatakayokupa msingi wa kujipanga kiuzalishaji ili hatimaye upate faida. Hivyo hata kabla hujaanza kuzalisha fahamu haya yaliyotajwa hapa juu.

(a) Kutafuta na kutumia taarifa za masoko ya sehemu tofauti:

Kwa kadri utakavyokuwa unaendelea kuzalisha, mabadiliko mbali mbali yatatokea kuhusiana na uzalishaji wako na hata kuhusiana na soko la bidhaa unayozalisha kwa maana ya kuku. Ili uendane na mabadiliko yanayotokea ni muhimu mzalishaji upate taarifa za hali ya soko mara kwa mara.

Taarifa hizi zitakusaidia kufanya maamuzi yatakayokuwezesha kuendelea kupata faida. Taarifa za masoko zinaweza kupatikana kwa wazalishaji kadhaa kuungana na kuunda umoja wao.

Katika umoja huo wawakilishi wachache wanakuwa na jukumu la kutafuta taarifa za masoko ya kuku sehemu mbali mbali ambako kunaweza kuwapa wazalishaji tija zaidi. Walio katika umoja huo watatumia taarifa hizo kufanya maamuzi ya kuuza kwa faida zaidi kwa pamoja au kwa mmojammoja kutegemeana na hali halisi. Watoa taarifa pia watafanya mawasiliano ya kuwajulisha wanunuzi juu ya upatikanaji wa kuku kwenye maeneo wanakozalishiwa.

(b) Mbinu zaidi ya kupata masoko mazuri:

(i) Umoja wa kuzalisha na kuuza;

Kwa kawaida kama bidhaa ina soko, wateja hupatikana kwa urahisi pale wanapohakikishiwa upatikanaji wa bidhaa kwa wingi katika sehemu moja.

Katika hali hii, wanunuzi huwa tayari hata kununua kwa bei ya juu zaidi kwa sababu ya kupunguza muda na gharama ya kutafuta bidhaa ya kutosha kupeleka sokoni. Kwa upande wa kuku jambo hili linawezekana kama mfugaji atafuga kuku wengi wa umri usiopishana sana kwa wakati mmoja. Watakapofikia kimo kinachofaa kuuza utawauza wengi kwa wakati mmoja na kwa faida zaidi. Mahali ambapo mfugaji mmoja mmoja hawezi kukidhi wingi wa hitaji la wanunuzi, wafugaji kadhaa wanaweza kuunda umoja wao wa kuzalisha (kila mmoja kwake ) na kuuza kwa kipindi kimoja na kupata faida zilizotajwa hapa juu.

Faida nyingine ya kuuza katika umoja ni kuongezeka kwa uwezo wenu wa kupanga na kusimamia bei mnayotaka kuuzia. Sauti na uamuzi wenu wa pamoja utawapa nguvu ya kusimamia bei yenu mnayoipanga dhidi ya bei za chini wanazotaka wanunuzi. Uwezo wako wa kusimamia bei unayoitaka ni mdogo ukiuza peke yako. Chama cha akiba na mikopo ni kikundi cha watu waliojiunga kwa hari yao kufanya ushirika wa kuweka akiba zao kwa pamoja na kutoa mikopo kwa urahisi kutokana na akiba zao. Kwa wafugaji wa kuku kibiashara wanashauriwa kuwa na chombo cha namna hii kitakachokuwa na utaratibu wa wanachama kuweka na pia wanachama hawa kuwa na fursa ya kukopa kwa lengo kubwa la kuendeleza ufugaji wao wa kuku kibiashara.Ufugaji wa kibiashara ungehitaji kuongeza mtaji mara kwa mara kulingana na mahitaji ya soko husika. Mfumo wa kuweka na kukopa utakuwa chanzo kizuri na cha kuaminika kukidhi haja ya mtaji endelevu kwa wafugaji wa kuku.

**Marejeo**


1. Heifer International Tanzania (2010) “*Mwongozo wa ufugaji kuku wa Asilia Wakulima Tanzania”*
2. Muzeza district council (…..) *“Ufugaji bora wa kuku wa asili na chotara”*
3. Rural Livelihood Development Company (RLDC), *“Biashara ya ufugaji bora wa kuku wa asili”*